Tuwe na hospitali ambayo inasaidia kila mwananchi wowote ambaye ni maskini na tajiri (inaudible). Mawasiliano iwe ikiwekewa mwananchi kwa sababu pahali kwingine hatuna barabara na hatuna njia yeyote ya kusaidiwa. Sana sana akiwa President amechukua Serikali ambayo ni ya chama fulani, vyama vingine wale hawakumpigia kura, hawapati mawasiliano yeyote. Hawasaidiwi na njia yeyote. Serikali inapanga budget na kila kitu.

Tuwe na maji kwa watu wote kwa vile watu wengine hatuna maji, tunaishi na tunasema tuko Kenya lakini wengine hata maji hatuna. Na huo ukulima wetu tunalima wote tungefurahia Serikali ijayo tuwe Soko huru. Vyombo vya habari viwe huru. Visiwe vikibagua hawa watu ni kabila fulani, ama ni wa chama fulani hawawezi tumia hivyo vyombo. Na ningefurahia kama tungekuwa na hati za kumiliki shamba.

Kwa sababu shamba nyingi wengine wengi hawana shamba. Kuna shamba zingine, hii nafikiri ni kitu moja ningeongea juu yake tungesaidiana juu ya mashamba haya ambayo tuko nayo, wengine wao wamekufa juu ya ukimwi. Sasa haya mashamba mingi na watoto wengi wamebaki huku na hata kulipa loan hiyo hawezi. Tungefurahia Serikali vitu kama hii iangalie. Iwe itaundwa kamati ya kuangalia vitu kama hawa wengine hawajiwezi. Na hawa watoto wameachwa kama yatima, wawe wakishughulikiwa, wapelekwe shule na Serikali isaidie ili tuwache kuwa na chokora wengi.

Yangu ya mwisho ningesema, Chief achaguliwe na wananchi. Asante.

Com. Bishop Njoroge: Can we have Ms. Dorris Wairimu?

Dorris Wairimu: My names are Ms. Dorris Wairimu and I am representing the staff of Utumishi Academy Gilgil. Our first recommendation is that, after the Presidential elections, if the President doesn't get over 50% vote, there should be runoff for the best two. Instead of taking the one with the highest votes and he could only have garnered about 20%.

Our next recommendation is that the MPs should not be allowed to award themselves hefty salaries. There should be a body outside Parliament, which discusses their salaries and not themselves. Then, taxes are too high compared to the cost of living and most of us are unable to live at least fairly. So, the taxes should be looked into and reduced if possible. Then representation

in Parliament should be equal. In other words, we have too many Members of Parliament and we need to reduce the number. That one can only be done if a Member of Parliament is given the same number of people to represent in Parliament like any other and our recommendation was that each MP should represent fifty thousand people.

Then, the President should not be the Chancellor of public Universities. This is because the Vice Chancellor is not able to function autonomously because he is answerable to the Chancellor who is the President. So, according to our view, the President should not be the Chancellor of public Universities. It should be left to the Senate to recommend and then the High Commission for Education to appoint a qualified Chancellor.

Our next recommendation is that the Parliament should vet top civil servants to avoid handshaking of people who do not qualify and people who have to thank a certain team. According to us, the Parliament should vet these people so that they can perform according to the expectations of everybody and not the person who has appointed them.

Our next one is on Local Authority: Our Local Authority has failed to perform in garbage collection and water supply. According to our observation, may be there is too much mismanagement. If they cannot deliver, we suggest that the Local Authorities be privatized. Then, we as teachers we observe that the Government has not been honest in its promises to the teachers and we recommend that in future, there should be honouring of what the Government has said it will do. In Gilgil, we teachers feel that it is an area under hardship conditions, may be it should also be looked into among other hardship areas.

Thank you.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much Dorris. Can you come Dorris and register here? Can we have Melvin Chiboli Melvin tafadhali? Tell us your names, your age and your class.

Melvin Chiboli: Thank you. My names are Melvin Chiboli, I am from Utumishi academy. I am eighteen years and in form four. To get to the point, mine is specifically about education. First of all, you find that there are less Universities. At least we are recommending that let's say from one University, we have Affiliate Universities like let's say Nairobi, you find like Strathmore be encamped to the J.K.U.A.T. or Jomo Kenyatta University. Because you find that many people pass but they cannot proceed because the spaces are less. We have found that the mean grades have been heightened to B. Which is supposed to be C+. So you find that there are many people who are not going on with their learning.

The second thing, also Universities should be equally distributed in all the Provinces. You find that let's say in Coast Province, they are only in Rift Valley and let's say Nairobi.

The other one was about the Children's Parliament. We were asking that the Government should not have any say in dismissing or building up the Children's Parliament. It should be done by the children themselves with the help of the Government just

guide lining it. Again, it should be equally represented from all the Provinces. To move out of education, we are also asking if the constituents themselves should have the mandate of passing a vote of no confidence to the MPs. Instead of leaving the MPs to do it which we have never seen.

You find that this let's say a constituency, the MP is not doing his work and he must remain for five years. So, we were asking if the constituents should have a say to pass a vote of no confidence to its MP. Again the other one was, free and compulsory education for children upto Standard four. You find that many homeless children let's say street children cannot learn because education is not free for them. Also, the system of education should be changed that is to meet the requirements of the current world. You see that we only go by the books and things like computer came, so many schools don't have these facilities which we are less fortunate to have. I think that is all I had.

Com. Bishop Njoroge: Thank you. Njoo hapa ujiandikishe. Duncan Githinji? Harrison Waweru? Paul Kamore? James Waka. Utamfuata huyu.

Harrison Waweru: Shukrani. Pendekezo langu ni ya kwamba, Rais na Mawaziri wasiwe Wabunge. Rais achaguliwe kutokana kati ya wengi ambao wamekuwa wakipigania kiti pamoja. Kukitokea namba moja na mbili, warudishane uwanjani ili tuweze kupata mmoja ambaye atakuwe akiakilisha nchi. Ardhi isimilikiwe na mtu binafsi. Zaidi ya ekari elfu mbili. Sehemu zingine za ardhi ambazo zilipiganiwa kutoka kwa mkoloni, ziachiwe umma. Kwa upande wa utawala ningependekeza Bunge, Mahakama na Urais vitenganishwe lakini ziwe zikitegemeana. Watumishi wa Serikali wasiruhusiwe kufanya biashara.

Elimu iwe ni bure kuanzia Primary hadi chuo kikuu. Serikali moja, sio Serikali ya Majimbo. Matibabu katika Kenya yawe ya bure. Upande mwingine ningependekeza sheru isiwe na mtu wa kubagua. Wengine wanaambiwa wanakuwa wanapendelewa na sheria na wengine ambao hawatembelewi. Waliopora mali ya nchi ningependekeza wasiruhusiwe tena kuwa watumishi wa umma na pesa ambazo wamepora kutoka kwa raia, Katiba iwalazimishe kurudisha. Katika nchi kuwe na Mahakama ya wazee. Uthamini wa vyama uondolewe pale, aliyepatiwa tikiti na chama, asiyajibika vilivyo. Bunge aondolewe tu pale, sitini na tano ya wapiga kura ambao walimchagua wanaona kwanza hawakilishi vilivyo. Kura ziwe zikihesabiwa mahali zilipigiwa. Kwa upande wa rushwa ningependekeza, iwe ni kosa la jinai katika nchi. Ningependekeza kuwe na mashamba ya Serikali ambayo yatakuwa yakichunjwa na Serikali ili kusiwe na upungufu wa (inaudible) katika nchi.

Uhuru wa kuabudu uheshimiwe kwa kila dini. Mali asili ilindwe kikatiba. Ardhi ya asili isihusike katika kile kifungu ambacho nilisema cha acre hamsini. Ardhi ya asili iwe vile ilivyokuwa kabla ya kupata uhuru. Mali iliyoibwa kwa Serikali irudishwe na wezi washitakiwe. Zile pesa wengine wanahamisha kupeleka nchi za ng'ambo zirudishwe virudishiwe umma. Ningependekeza walimu wakuu wa shule wasiwe makarani wa kuandikia wanakamati. Mwalimu awe ni Mwalimu tu, asihusike na kamati ya shule.

Madaktari wawe wakiajibika kufanya kazi zao. Wasiwe na ma-clinics zingine kule na kule na dawa wanachukua wanapelekwa kule. Katiba ikataze hiyo kabisa. Ma-Councillor wasiruhusiwe kumiliki mali ya Council wakati wanapohudumu.

Mwisho ningependekeza ndoa zihalalishwe Kikatiba na kuwe na uhuru wa kutengana iwapo kumetokea hali ya kutosikilizana. Ni hayo tu.

Com. Bishop Njoroge: Asante sana. Utakuja ujiandikishe pale. James A. Waka. What we need is just highlight points. Five minutes.

James A. Waka: Thank you. My name is James Waka. I am a resident of Gilgil and at the same time a businessman. These are my points, the Commissioners:

Political parties: We have too many in Kenya, this should be restricted to the maximum of five political parties because some of the political parties are just for commercial purposes and some are of ethnic grouping.

Two, the Members of Parliament are not on permanent and pensionable jobs. It is a contract, therefore, they should not decide over their salaries and other benefits.

Three, our country Kenya has been eaten up with a lot of corruption and looting of public funds. Looting of the Government resources. This should be punishable and taken into consideration as treason.

Four, the President should not be above the law and the President can be tried in any law courts or the highest law courts of the land. In case, the President has mis-used his office or has deliberately shown evils like corruptions, nepotism and so on.

Five, Local Government, in Kenya we have seen a lot of corruption, land grabbing, mis-appropriation of public funds, taking even the land for political....

Com. Bishop Njoroge: Give proposals.

May I propose that, if that continues the Review Commission should recommend the Local Government to be scrapped and probably be replaced by a Provincial Administration. Whereby the Provincial Head or Administrator is elected by the public or the voters.

Six, Public Service Commission. With the Public Service Commission, it has already a lot of nepotism, tribalism and then many Kenyans end up without employment. May I say, the Review Commission address on this particular issue very strongly. That

any Public Service Commission found of such evils be removed from his employment.

Number seven, nomination members of Parliament and nomination members of the Local Authority. This should be restricted to one term of the office. That is five years of the office for life.

Number eight, all board members of the departments may be educational boards, roads board and so forth. The people or the personnel manning those particular boards should be elected and not nominated.

Last, I had many but the fact that time is running out, I am giving my last recommendation. Which is number ten. Unitary Government has seemed to have failed Kenyans. More than twenty years during the colonial rule. Forty years during these particular years. May I recommend that we have the structure of Government which is very serious on development matters. A President with a Deputy President. Government with a Prime Minister who is in charge of day to day running of the Government and the Government which is free without evils like greed, corruption or bribery, nepotism, mis-use of powers and looting of the public funds. Eight other Vice Presidents be elected by voters in each and every Province to be incharge of the development lines on each and every Province. Thank you.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much. James K. Thuita? Mzee utajiandikisha pale.

James K.Thuita: Commissioners and observers. My name is James K. Thuita. Ya kwanza ningeeonea kuhusu kazi, especially kazi kama ya jeshi, nurses, teachers, tumekuja kuona kwamba hizo ni kazi ambazo zinapatikana na walio na pesa na wale wako kwa ma-towns. Wale wako mashambani wamesomesha watoto wao hawana nafasi ya kupata zile pesa.

Com. Bishop Njoroge: Kwa hivyo unapendekeza nini?

James K.Thuita: Recommendation ningeeona in every sub-location ama location kuwe kunachukuliwa wale watu wanatakikana wapewe kazi. On the other hand, mambo ya prisoners. Kama mtu sio mhalifu vile na amefungwa more than two years and above, awe akipata nafasi ya kutembelewa na bibi yake. Ili marriages zizivunjike. Prisoners rights.

Number three, tuongee mambo ya farmers. Serikali ilinde ukulima. Tumeona uchumi wetu umeharibika sana. Ilindwe sana especially watu wa farming waangaliwe.

Number four tuingie mambo ya President. Wakati Bunge limevunjwa kama President Moi, awe anapewa gari yake asitumie gari za Serikali ama any administration. Awe raia wa kawaida. Before amerudishwa katika kazi. On profession, I am a tailor. Haki kati ya wale nafanyia kazi. Ningeeonea sana. For instance, niko na mtu, ameenda amegonjeka and for three months hajaonekana. Zile rights za kukuja kusema nina haki yake niko nayo. Na mimi nasema wakati umepita. Kuwe na sheria

inasimamia my clients, mteja na mimi.

Ya mwisho ningeonea kuhusu church, freedom of worship. Hii uhuru wamepewa wengi wamekuwa si freedom. Katika area yetu wengi wanapiga duru sana usiku. Hata kuingia huwezi. Huwezi elewa wizi uko pande gani juu church imekuwa nayo, imekuwa na a lot of disturbance. Ni mzuri church tunaipenda na ni yetu. Lakini at least kuwe na limit.

Ya mwisho tuongee kuhusu Attorney General. Awe ni mtu wa kuchaguliwa. Asiwe ni mtu appointed. Second, education i-remain kama zamani. Thank you.

Com. Bishop Njoroge: That is 7-4-2-3. Haya tumpate Joseph Ole Lishinga, anasimamia wale wengine. Karibu Joseph.

Joseph Ole Leshinga: Ashe along.

Translator: Basi asante sana.

Joseph Ole Leshinga: Chairman Commissioner

Translator: Ma-Chairmen na Commissioners,

Joseph Ole Lishinga: Ore embae ai e dukuya,

Translator: Swali lake la kwanza.

Joseph Ole Lishinga: Kore enkarna naa kaaji Joseph ole Leshinga

Translator: Jina langu ni Joseph Ole Leshinga.

Joseph Ole Lishinga: Ore empae ai e dukuya,

Translator: Swali langu la kwanza,

Joseph Ole Lishinga: Naa peishoruni ena katiba etaata serkali oo ngutot.

Translator: Kwa wakati huu Serikali ile tunataka kwa Katiba wakati huu tunataka Serikali ya Majimbo.

Joseph Ole Lishinga: Enkaraki ore tena kop nikitii e Kenya nera nkabilani naatii artam aare.

Translator: Kwa sababu makabila yetu ya Kenya ni makabila arobaini na mbili.

Joseph Ole Lishinga: Naa ore kuna abilani kutiti nemitum aikata erishata teneguluni orasi amu ore tena kena naji keeta iltunganak ukabila,

Translator: Tunaona ya kwamba ikiwa kama ni wakati wa Uchaguzi wa Rais, hizi makabila ndogo ndogo hakuna nafasi ya kupata Urais.

Joseph Ole Lishinga: Neaku pee eishoruni taata tena rishata ina serkali e majimbo.

Translator: Kwa hivyo kwa wakati huu yeye anataka Serikali ya Majimbo.

Joseph Ole Lishinga: Ore enkae eare,

Translator: Swali lake la pili,

Joseph Ole Lishinga: Naa enapa sheria musana naitasheiki iljambai,.

Translator: Ile sheria ya kwanza ya first registration ya Title Deeds itupiliwe mbali,

Joseph Ole Lishinga: Pee egili ina sheria nenangari amu kearita ninje iyiook kira Ilmaasai.

Translator: Hiyo sheria ifutiliwe mbali kwa sababu ilikuwa kitu cha ukoloni.

Joseph Ole Lishinga: Ore namba uni,

Translator: Namba ya tatu,

Joseph Ole Lishinga: Naa land board.

Translator: Land Control Boards,

Joseph Ole Lishinga: Ena naitasheiki oldioi (DO) iljambai metimiri neaku oljamba leitu enyorra iltunganak metimira oltungani

neimie oldioi teneishori ropiani.

Translator: Ile kamati ya kukaa huko kwa ofisi ya D.O., hawa wakupitisha mashamba kuuzwa, hiyo hatutaki kabisa.

Joseph Ole Lishinga: Pee eitasheiki loopeny iljambai lenye.

Translator: Isimamiwe na wenyewe. Wale watu wa klasi ya chini huko.

Joseph Ole Lishinga: Ore namba onguan,

Translator: Namba nne, Kenya imejitangazia imenyakua uhuru.

Joseph Ole Lishinga: Naa kulo shambai apa kitejo ore taata nikijo kiata uhuru,

Translator: Lakini jamii zingine zingali hazijapigania uhuru zingali zinatarajia uhuru utapatikana.

Joseph Ole Lishinga: Kake tenikidol iyiook kira Imaasai nikidol anaa emikiata uhuru.

Translator: Kwa sababu kutoka Naivasha mpaka Nakuru.

Joseph Ole Lishinga: Amu ore teininteru kutoka Naivasha mpaka Nakuru,

Translator: Ni shamba ya watu wawili tu ndio iko.

Joseph Ole Lishinga: Naa iljambai loo iltunganak waare ake oti.

Joseph Ole Lishinga: Naa tinidung lelo shambai aatua nikimpungi, nikingori, neibungi ngishu, neikenori.

Translator: Hayo mashamba hata ng'ombe yako ama mtu kukanyanga anapigwa risasi ama saa ingine anafungiwa kama hapa Delamere.

Joseph Ole Lishinga: Kiata ngishu nikinosa olkesi olari musima.

Translator: Tuko na ng'ombe tumefanya kesi mwaka mzima.

Joseph Ole Lishinga: Etomito iltunganak tenkaraki netijinga apa oljamba.

Translator: Watu wakiwa wamezuia ng'ombe kwa sababu zilikuwa zimeingia shamba lao.

Joseph Ole Lishinga: Paa tiaji kiata uhuru aa enkop ang kiimita naa ninye eimita ngishua ang neibungi iyiook?

Translator: Kwa hivyo uhuru bado haujafika kwa sababu ungali bado unazuiliwa.

Joseph Ole Lishinga: Ore enkae bae ene,

Translator: Swali lake la tano,

Joseph Ole Lishinga: Naa National Parks

Translator: Hizi national parks ama sehemu hizi za wanyama.

Joseph Ole Lishinga: Ore iyiook kira Ilmaasai kiboitare iyiook inguesi.

Translator: Sisi jamii ya Wamasai tunaishi na wanyama.

Joseph Ole Lishinga: Nikitii nena Parks.

Translator: Na tunaishi karibu na ma-parks hizo.

Joseph Ole Lishinga: Naa tenejing ngishu ang Park neibungi iyiook.

Translator: Na ng'ombe kuingia tu kwa waya ya national park,

Joseph Ole Lishinga: Naa tenepuku nena nguesin nenyanya iljambai lang.

Translator: Na hao wanyama nao kutoka kuja sehemu ya reserve,

Joseph Ole Lishinga: Naa tenepuku nena nguesi, near ilturo lang,

Translator: Na hao wanyama wanaingia kwa makao yale yao,

Joseph Ole Lishinga: Naa tenepuku nena nguesin neaki ngishu ang emueyian.

Translator: Na hao wanyama wanaleta kupe nazo kupe zinaambukiza ng'ombe ugonjwa.

Joseph Ole Lishinga: Near iltunganak nemetta entoki nalakitae.

Translator: Na inaua watu na hakuna kitu mtu analipwa.

Joseph Ole Lishinga: Eitodolu ajo hasara egira ayaaki ninje iyiook nena nguesin etii nkuapi ang.

Translator: Kwa hivyo wanyama inaonekana wanaletea sisi hasara.

Joseph Ole Lishinga: Neaku ai kiyieu nelaki iltunganak lang tenenya nena nguesin,

Translator: Wale watu wetu wanauawa na hawa wanyama ama mwananchi yeyote wa Kenya akiuliwa na mnyama,

Joseph Ole Lishinga: Nelaki sii ilturor teneat oo iljambai tenenya

Translator: Na alipwe zaidi ya milioni tano badala ya elfu thelathini.

Joseph Ole Lishinga: Ore 70% enena ropiani, nepuo ina shoto oo Ilmaasai pee eisumieki nena kera amu ina kop etii nena nguesin.

Translator: Na communities za area hizo national parks ziko, walipwe seventy percent.

Joseph Ole Lishinga: Ore sii taata anaa taata nene wuejitin niko forest,

Translator: Forests,

Joseph Ole Lishinga: Keyieu sii ninje neingori iyiook kira iltunganak loo ngishu.

Translator: Tunataka nao upande wa wafugaji wa ng'ombe iangaliwe.

Joseph Ole Lishinga: Metaa ore te nkata o lameyiu neishori iyiook nena forest meinosa ngishu.

Translator: Kwa wakati wa Kiangazi, sisi turuhusiwe kufuga ng'ombe katika forests. ‘

Joseph Ole Lishinga: Ore enkae bae ai e mwisho,

Translator: Swali lake la mwisho,

Joseph Ole Lishinga: Naa taata esiai taata anaa esiai e Kanisa.

Translator: Mambo ya kanisa.

Joseph Ole Lishinga: Ayieu naomonu paa ore tenakibelegenyata ena katiba e taata,

Translator: Anataka kama marekebisho ya Katiba iko sasa,

Joseph Ole Lishinga: Pee eishori Kanisa engolon, naitasheikinye naaji emoruua.

Translator: Kanisa ipewe nguvu kabisa iwe inasimamia usalama katika area zote kwenye kanisa iko.

Joseph Ole Lishinga: Tenkaraki pee ingor ajo ore kulo tunganak ooji ilmukurani naa atua iyiook etii,

Translator: Kwa sababu tunaona wakora wako ndani yetu.

Joseph Ole Lishinga: Naa ore kila emoruua keyiolo iltunganak oltungani torono.

Translator: Na kila sehemu ama kila villager anajua watu wake sawasawa.

Joseph Ole Lishinga: Nemeyiolo sikarini, nemeyiolo kotini.

Translator: Na askari haijui na korti haijui.

Joseph Ole Lishinga: Naa ore kulo tunganak le kanisa naa kedup aatayiolo ninje neaku teneot ilo tungani neirusuni ilo tungani mewai kabisa nemeeta board.

Translator: Basi wazee wa kanisa waki-point mtu ya kwamba yeye ni mwizi katika area hii yetu, ichukuliwe maanani na

afungwe miaka mingi.

Joseph Ole Lishinga: Tenkaraki kidol ilo tungani aajo, lelo tunganak oomiti iyiook kipuo dukuya.

Translator: Kwa sababu hizo groups za wezi ndio wanatusumbua sisi wote.

Joseph Ole Lishinga: Amu atua naa iyiook etii naa keitayu ropiani aihongisho.

Translator: Na wako ndani yetu na polisi hawawezi kuwashika.

Joseph Ole Lishinga: Nee meeta enaiko pee eihonka irpayiani le Kanisa.

Translator: Na hawezi omba wazee wa kanisa,

Joseph Ole Lishinga: Naa ina kata ake kintau iltunganak torok ti atua moruuak.

Translator: Ndio hiyo tutamaliza wezi ndani ya location ama village.

Joseph Ole Lishinga: Naitabaiki ine wueji,

Translator: Na amesema asante sana, amefikisha hapo.

Joseph Ole Lishinga: Natejo sii pee irinyokini iltunganak iljambai lenye.

Translator: Na watu warudishiwe sehemu zao.

Com. Bishop Njoroge: Asante sana kwa hayo maoni. Paul Njamba?

Paul Njamba Karanja: Kwa majina ni Paul Njamba Karanja. Maoni yangu ni kama yafuatayo:

Kuapishwa kwa watumishi wa Serikali: Jambo hili nafikiri hata ndio maneno ya kugeuza Katiba ipatikane, ni kwa vile watumishi wa Serikali hawazingatii, na hawazingatii kwa kutojua, wanazingatia kwa kupuuzua. Kwa hivyo mapendekezo yangu naona jambo hili la kuaapisha na kitabu kitakatifu cha Biblia ambacho hawakiheshimu, maana wengine ni makafiri, wengine ni waomba sanamu, wengine ni wa kanisa la devil worshippers. Kanisa ipewe uhuru wa kuendesha Serikali na Serikali ibaki ikiwa Serikali. Kwa hivyo iapishe na jinsi wanavyopendekeza wenyewe. Kwa maoni yangu mwenyewe...

Com. Bishop Njoroge: Unasema hivi, watu wasiapishwe tena na Biblia. Kwenda kwa pointi ingine.

Paul Njamba Karanja: Waapishwe na ishara ya adhabu ambayo kwangu mini mwenyewe naona ni pingu.

Ya pili, uteuzi wa watumishi wa Serikali, kama vile wanajeshi, askari wa utawala na askari yeyote yule ambaye ni mlinda usalama. Hii ina maana kuwa, maofisa wanaochukua ama maofisa ambao wako Serikalini, viongozi wa wanajeshi na wengineo. Sisi raia tunawalaumu kuwa ni kama hawazingatii kazi yao. Maanake katika Serikali tunapata D.O. wanatumia bunduki zao na askari kwenda kupeana hizo bunduki kwa wezi wenzao. Kile kitu kiko, kwa maoni yangu mwenyewe ni kabla ya vijana kuteuliwa, kufikishwa kwa ule uteuzi, kwanza wateuliwe katika ofisi ya Chief ambaye ndiye anawaelewa. Anajua wakora, lakini sio kutumia pesa au kuangalia masura kama wakati wa mkoloni.

Ya tatu, sheria itakayolinda vyama vya kisiasa na pia iwe italinda mwananchi wa kawaida. Kwa mfano, mtu asitoke kwa chama hiki na kwa muda wa mwaka huo huo, aende tena aunde chama kingine. Jambo hilo ndilo linaleta mambo ya clashes katika taifa letu. Mbunge pia akihama chama, asipigane Ubunge kwa miaka mitano.

Vyeti vya ndoa: Vyeti vya ndoa kwa maoni yangu mimi naona viwe vikitolewa baada ya miaka mitatu. Hii italinda njia ya kuvunja ndoa ovyo ovyo. Au ndoa za kusahihishiwa na mtu. Kwa hivyo mtu atakuwa akipewa cheti cha ndoa baada ya miaka mitatu kwa hivyo atajua kuna jambo fulani litakalofanyika baada ya miaka mitatu. Atalinda ndoa yake.

Com. Bishop Njoroge: Uko karibu kumaliza?

Paul Njamba Karanja: Ndio. Uhuru wa teknolojia uwe uko. Hiyo sitaelezea sana.

Ya sita, Serikali kuchukua maoni ya wananchi mara tu baada ya janga la kitaifa kutokea. Serikali ichambue kisha waichapishe kwa gazeti la kitaifa na redio za kitaifa. Hiyo ni maoni ya wananchi kupokelewa baada ya janga la kitifa kutokea.

Ukahaba uhalamishwe katika taifa letu.

Com. Bishop Njoroge: Hiyo ni kusema nini?

Paul Njamba Karanja: Ukahaba uwe ni marufuku kabisa katika taifa. Jambo hili pia limeharibu taifa kabisa na hata taifa letu tukufu kukosewa heshima mpaka nchi za kigeni. Ukahaba huu ndio umeleta janga la kitaifa ambao ni ukimwi. Pia ukahaba ndio uti wa mgongo wa maovu, kama vile mipango ya jambazi na pia uvujanji wa ndoa na kuweka kiwango cha elimu kuwa cha chini.

Com. Bishop Njoroge: Hiyo tumepata. Ungetaka hao wafanye nini iliwaweze kuishi maisha yao?

Paul Njamba Karanja: Makahaba. Ndio tunatafuta kazi kwa Serikali.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much. You have very original ideas, hatujaambiwa na mtu mwingine. Francis Kanyi. Okey.

Francis Kanyi: Thank you Chairman, the other Commissioners and my colleagues here. Kwanza ningetaka kusema pole kwa mwenzenu ambaye pia ni mwenzetu, kutuacha Bwana Ombaka pole sana. Yangu ingawa yamesemwa, nitasema kwa ufupi. First, even if you can be able to do that, this evening. Can you first underline that phrase, President to be above the law. Hiyo iwe imefutwa kabisa. Because this one, has made the President to appear like a God to the politicians and some of them have adapted calling the person as 'mtukufu' na ikawa ni kama dini. Karibu kumuabudu na ni makosa.

Ya pili, the President must be thirty five years and above lakini hatujajua ni wakati gani anafaa kutoka kulingana na Katiba. Ikiwa unafanya kazi katika kiwanda fulani, kufika jioni, you will be a suspect in the same factory. So, if you overstay in a place, I think you loose the relevance. Napendekeza...

Com. Bishop Njoroge: Can you just give us mapendekezo please?

President to be thirty-five years and above and on attaining sixty nine years, when he is celebrating sixty nine years, he should leave office even if he is the incumbent President. Even if he is the serving one he should retire at that age. There should be two terms for a President, who should be qualified at least one at a degree level. That is somebody who is knowlegable and able to manage the affairs of a country like Kenya. Kenya must stop having tribes in their identity cards or anywhere as an identification factor. We should have a tribe as Kenyans. Then the other tribes should remain the way people are and we respect one another. Those are just languages, geographical languages, we have a tribe Kenya. Parliament to appoint senior Government employees like Permanent Secretaries and Parastatal Heads. Mayors, Vice President to be elected as well. One man, one job. We have an employment problem but we have a person with about ten jobs. How can we solve this unemployment problem?

Com. Muigai: Usiongeze chumvi. Mwalimu usiongeze chumvi. Umesema one man, one job, tumeelewa sote ni kusema nini.

Francis Kanyi: Education for all. Na ihakikishwe watoto ambao hawawezi kupata nafasi ya elimu ni jukumu la Serikali kuwaelimisha kwa sababu mzazi wake pia hajiwezi na jukumu la Serikali ni kutumikia wananchi wake.

Mwisho ikiwa Serikali inaajibika katika nchi, inafaa kuangalia sehemu zote. Sehemu kama inawakilishwa na Mbunge wa

upinzani au wa chama kinachotawala. Itakuwa ni makosa, kuacha sehemu ambayo inawakilishwa na Mbunge wa upinzani kwa sababu ni mpinzani. Lazima yote iwe equally attended. Kiongozi wa nchi aweza kushtakiwa ikiwa kuna evidence ya negligence.

Thank you.

Com. Muigai: Thank you very much. Chief Kariuki yuko? Hayuko. Simon Murimi. Afuatwe na Charles Mureithi. Charles Mureithi yuko? Kuja hapa mbele Mzee. Silas Wahome. Uko. Karibia hapa na Wilfred Kadagwala. Mketi hapa mbele ndio tuonane. Endelea Mzee.

Simon Murimi: Thank you Chairman, Commissioners and attendants. My name is S.M. Murimi and I am a businessman in this area. I would like to recommend to this Commission that land ownership should be respected and protected by the Government. I have in mind cases of land clashes or collisions by; we have these people who are nomadic grazers and they take their cattle to every place. In that they clash with the owners or the locals of that area. So, I would recommend that a way should be found so that when we have famine and we don't have rains, these people should reduce their animals or take them to K.M.C. Even if K.M.C has grounded, it should be rehabilitated.

Elections should be held after every five years regularly and preferably it should be held sometime from 1st to 20th of December. That the present five-year term limit for the Head of State should remain so. But then age should not be a factor to bur somebody from continuing as Head of State. When one has not reached the limit of two terms, he can still continue.

The other point is, that Local Authorities should be established to give services to the locals but not to be supported by locals without service. That land owned by Local Authorities should not be given without the authority of the Local Authority or the local leadership.

There are cases where we have especially let's say like Gilgil or elsewhere, we have people coming from Nairobi, giving out land without the knowledge of the local people or the Local Authority or the local leadership.

That employment to Government departments like Armed Force, Police Force and others should be based at least on proportion to population. We have cases where we have some tribes like El-moro having employed people in the Army may be upto a thousand and when we come to a big tribe like Baluhya, we have only one hundred. So, I think I was trying to say. That's all.

Com. Muigai: I want to ask you one question relating to land. You say when local land is being allocated, the local people must be involved. I want to ask you a question about the office of the Mayor. The people who do the allocations are the officers, town clerks, treasurer, engineer and so on. But they are sent to.....

Second question would you like the Chief officers to be appointed by the Ministry or hired from the grassroots.

Simon Murimi: I beg your pardon. The second question is?

Com. Muigai: The Chief Officers, the town clerks, the treasurer, they are appointed from Nairobi and then sent to Naivasha. You understand my question? Would you like them to be hired directly by the Councillors themselves and the Mayor or would you like them to come from Nairobi.

Simon Murimi: The first question, I would recommend that the Local Authority hires such officers directly from whatever quarter. There was the first one may be I have forgotten.

The first one was about the Mayor, you know the Mayor is elected by Councillors for two years? We have received some recommendations that the Mayor should be elected directly by wananchi. I wanted to hear your views on that.

Simon Murimi: My recommendation is, Mayors should continue being elected by the Councillors because otherwise we will need to have another post for that seat. Because they are supposed to come from the other Councillors.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much. Can you come and register? Paul Ole Lapio.

Paul Ole Rapio: Ashe oleng Bwana Commissioner.

Translator: Asante sana Commissioners.

Paul Ole Lapio: Ore too nkarna ainei naa kaaji Paul ole Rapio

Translator: Kwa majina anaitwa Paul Ole Lapio.

Paul Ole Lapio: Ore embae ai e dukuya naimaki tene wueji,

Translator: Ile kitu cha kwanza nataka kuzungumza kwa wakati huu.

Paul Ole Lapio: Naa kaisho Enkai enashe ninye taata kietuo iyiook ene wueji neimakinieki esiai e katiba.

Translator: Narudishia Mungu shukrani kwa kutupatia nafasi ya kuja kuwa pamoja.

Paul Ole Lapio: Amu ore apa katiba apa natulusoyie naitoroki te Kenya to laarin artam.

Translator: Kwa sababu ile Katiba iliyokuwako ile iliyokuwa imepita miaka arobaini baada ya kutungwa,

Paul Ole Lapio: Naa eikuti apa Ilmaasai oleng otii, ooshomo ene wuei.

Translator: Raia wote wa Kenya walikuwa wachache sana wale walioshiriki.

Paul Ole Lapio: Neaku ore embae naimaki tene,

Translator: Kile kitu anazungumzia,

Paul Ole Lapio: Naa e siai orkuak lang,

Translator: Ni mambo ya culture.

Paul Ole Lapio: Etii iltunganak longira iatumia orkuak lang oleng.

Translator: Hatutaki watu wengine watuige kwa mfano culture ya Wamasai.

Paul Ole Lapio: Amu kegira apuo aamor iyiook taata aitumia vibaya.

Translator: Anasema wale wengine wanatumia vibaya.

Paul Ole Lapio: Neaku kayieu taata neimieki tena katiba,

Translator: Kwa hivyo nataka kwa Katiba hii mpya.

Paul Ole Lapio: Nepiki sheria metaa ore engae abila pookin neitumia orkuak lenye.

Translator: Kila Mkenya atumie mila yake.

Paul Ole Lapio: Amu etii iltunganak loo loreren oogira oleng aitumia orkuak aaponu aifaidika te ilo kuak.

Translator: Kwa sababu makabila mengine yanataka kuharibu mambo ya wengine.

Paul Ole Lapio: Ninepu oltungani eishora entoki torono oleng namor iyiook.

Translator: Kwa sababu wengine huchonga watu wakiwa uchi.

Paul Ole Lapio: Nikidol ajo mee entoki sidai ina oleng.

Translator: Na tunaona hiyo si mzuri.

Paul Ole Lapio: Ore enkae e are,

Translator: Kile kitu cha pili,

Paul Ole Lapio: Naa esiai oo ngiri.

Translator: Ni mambo ya nyama.

Paul Ole Lapio: Ore oshi iyiook Ilmaasai naa ngiri, entoki naji enkiteng gintegemea.

Translator: Anasema sisi tunategemea nyama,

Paul Ole Lapio: Naa ore enkata naimakini esiai anaa budget te bunge,

Translator: Na wakati tunakuwa na siku ya kusoma budget,

Paul Ole Lapio: Nemeimakini aikata esiai oo ngiri.

Translator: Mambo ya nyama haizungumzwi,

Paul Ole Lapio: Eimakini kulie tokitin kake kegirori nena.

Translator: Na vitu vingine vinapandishwa, na vingine vinateremshwa na nyama haipandishwi na ni pesa mingi sana.

Paul Ole Lapio: Naa ore tenakata pee kimpang pookin tene wueji,

Translator: Sisi wote kama tunatoka kwa hii nyumba,

Paul Ole Lapio: Nining oltungani ejoki oltungani le butchery tudungokoki enkiringo nepir.

Translator: Sisi wote tunakimbia kwa butchery kutafuta nyama choma ile tayari na ile ingine inapimwa.

Paul Ole Lapio: Neaku kayieu neinguraa katiba ina siai,

Translator: Kwa hivyo Katiba iweke ya kwamba, ng'ombe ama wafugaji wote watafutiwe nafasi katika nchi.

Paul Ole Lapio: Pee etum sii ninje ngiri aanoto bei.

Translator: Nyama iwekwe katika budget ya nchi.

Paul Ole Lapio: Neaku nena nainei.

Translator: Na yake ni hayo.

Com. Bishop Njoroge: I think that is sensible. Charles Mureithi. Akifuatwa na Silas Wahome.

Charles Mureithi Kagiri: Majina yangu ni Charles Mureithi Kagiri na yangu itakuwa na machache sana. Ya kwanza ile ningeonelea kwa sababu wakati tuko hapa, tungetaka tuelewe kile kinachotakikana na Katiba na unatakiwa ueleze kile kitaandikwa pale ili kesho ikienda iwe ni Katiba inazungumziwa na inawekwa kukulinda na njia yeyote umesema. Yangu ya kwanza vile nimeonelea ya maana sana, ni nyinyi Wana-Commissioners, ningetaka muandike kuwe na skuli kwanzia kwa wakati Serikali tunayoenda kupata wakati huu. Hiyo skuli iwe ni ya kufundisha mwananchi wa kawaida vile anaweza kuishi nchi yake. Kwa sababu sisi tunaishi nchi yetu kama wanyama wa msituni. Kwa sababu, yeyote akiwa ni kiongozi, akiwa ni polisi, akiwa ni mtu wa aina gani, bora tu awe ameajiriwa mahali, akienda akute mwananchi wa kawaida ambaye hata hajasoma, haelewi ni nini, anamtunikisha. Kwa sababu ni mjinga. Kwa hivyo ningewauliza muandike Serikali itakayokuja iwe na skuli ya kufundisha mwananchi Katiba ya kuishi nchi yake.

Ya pili, President atakayekuja sababu ninaelewa kupata President mpya, wakati unaowadia. Awe ni chairman wa Bunge. Ikiwa kuna shida yeyote ya nchi, aite Wabunge na Ma-Ministers waje awaeleze, kuna shida hii. Waongee waongee, wakipitisha Wabunge wote, wapitisha. Yeye awe ni Chairman wa kueleza vile wameelewana. Lakini sio kuweka nchi mfuko wake kama kitambaa ya makamasi. Hiyo ni ya pili.

Upande mwingine, tunaolewa ya kwamba, katika nchi yetu, hakuna mtu yeyote ana uwezo wa kusema kitu ama kuendesha kazi yake. Hata ukiwa ulisomeshwa na baba yako, hata ukiwa ulipata degree kumi, hizo zote degrees zako ni za bure. Kwa hivyo ningepuliza Ma-Commissioners waandike, yeyote atakaye ajiriwa na ana masomo ya kulingana na kazi ameajiriwa, akubaliwe aendeshe kazi yake kihari. Iwe ni Katiba. Eti huyu mtu ataendesha kazi yake vile ajiriwa kulingana na masomo yake. Lakin sio tu akianza kidogo, simu inakuja, degree yake yote anaweka kwa cupboard. Tunakataa hiyo.

Hivyo ni kusema, kwa upande wa defence, kuna defence. Kama sasa unaweza kusikia kuna mtu ambaye amesoma ameenda ng'ambo na hayo yote yamefanywa na wazazi wake. Wametumia muda mwingi, hata kuenda bila viatu, hata kwenda bila nini, kufundisha mtoto ajitegemee ya kwanza. Mtoto wangu akisoma na akiwa na vyeo kama hivi vyote, mwishowe mimi nitakula na kijiko. Alikuwa akikula na mkono, akifikiria akifundisha mtoto na nini, atakula na kijiko. Baada ya kufanya hayo yote anakuja kuchukua jembe kuchimba mtaro. Na ni masomo yake. Kwa hivyo mwananchi wa kawaida yeyote aliye katika Kenya, mahali ako, awe akifikiriwa. Mtoto amesoma kama miaka hapo mbeleni, tulikuwa tukiambia.

Com. Bishop Njoroge: Pointi yako ni kuwa waliosoma wapate kazi.

Charles Mureithi Kagiri: Kupata kazi.

Com. Bishop Njoroge: Enda pointi ingine.

Charles Mureithi Kagiri: Ya pili, kuajiri Ma-Ministers, sio tu kutafuta Minister, mtu anachimba huku msituni, unakuja unampatia Minister. Na mahali hapo kuna watu wamesoma. Wanaweza kuendesha kazi, wanaweza kuendesha nchi kwa kila njia. Mtu mwingine kama mtu mwingine anachimba huko kwa mtaro, anachimba huko kwa mtaro, anapima mtama anachimba. Panda mbogo, anafanya nini. Ukimwambia umpatie book ya Agriculture atajua ni kitu gani unampatia?

Com. Bishop Njoroge: Kwa hivyo kila Minister apewe kazi?

Apewe kazi kulingana na masomo yale amesoma. Kwa sababu kuna Ministries na hizo Ministries yote, na watoto wamesoma na wako na masomo haya. Wapewe kazi kulingana na hivyo.

Ingingine yangu, Mbunge akiwa na shida ama akufe, President hana ruhusa ya ku-nominate Mbunge aende Bunge. Ameenda kufanya nini? Na hali sisi tuko na sisi tunawachagua waweze kulinda Constitution yake. Wewe una-nominate Mbunge, anaenda kutuakilisha nini? Unaweza ku-nominate Mbunge hata bubu na haoni wale wanaongea katika Bunge. Tunataka arudishwe mpaka kwa sisi. Tumchagua aende directly Bunge, tukiwa tunamchagua. Ili akikosea anarudi kwetu.

Com. Bishop Njoroge: Nataka kusahihisha. Wabubu, kuna wabubu wao. Sawasawa? Kwa hivyo kila mtu ana haki ya kusimamiwa na hakuna mtu hana haki kwenda Bunge hata kama hajui kusoma au haoni. Sawasawa? Inginge, ya mwisho.

Kwa hivyo...nilikuwa nikisema Mbunge akiwa na shida ama kuwe kiti yake imeachwa wazi, itangazwe, ifanyiwe uchaguzi ili akienda Bunge awe ni sisi tunamchagua.

Inginge sasa ambayo ningesema, huku katika Kenya yetu tuna shida na ingetakiwa Katiba iundwe na kuwe na kamati ziko katika locations, division, district, kuwe na command imeundwa na Serikali ili kamati hiyo, kukiwa kuna shida, yeyote ya chama, wanaanzia pale grassroot kwa kufikiria hiyo kesi. Badala ya mtu kwenda kukumwambia, 'wewe tutaonana.' Sababu anaelewa ofisi ataenda, wewe ukiingia huko utafukuzwa. Ndio anakuambia mtaonana. Kwa hivyo Wazee wa location, division hawatakuambia tutaonaona. Watafikisha hiyo kesi na ile barua wataandika itachukuliwa vyema na suluhisho itapatikana. Yangu imekwisha.

Com. Bishop Njoroge: Asante sana. Njoo ujiandikishe hapa. Silas Wahome. Yuko hapa?

Silas Wahome: Jina ni Silas Wahome. Pendekezo langu la kwanza ni kuhusu hali ya uhuru wa kuabudu. Pendekezo langu ni kwamba katika mashule, watoto wetu wawe wanasoma kuanzia jumatatu mpaka siku ya ijumaa. Lakini zaidi kuna wengine ambao wanaweza kusoma siku za weekend. Hivi kwamba kuna watoto wengine ambao hawapati nafasi ya kuweza kuabudu Mungu kwa vile mitihani ni nyingi ama masomo mengine yamewekwa katika siku za weekend. Ingekuwa tutaweza kuwa na uhuru wa kuabudu, pia na watoto waweze kupatiwa uhuru wa kuweza kuabudu hata siku ambazo wanafaa kuweza kuabudu.

Ya pili ni kuhusu hali ya kulinda mali ya umma. Ikiwa ni ushuru ambao unaotzwa katika upande wa wafanyakazi yaani kodi ambazo zinatozwa wana-biashara ziingie tu katika sehemu zinazohitajika. Hivyo kwamba zisichukuliwe na vote nyingine. Kama ni upande wa County Council wamepewa ushuru wa kukusanya takataka ama vitu vingine, iingie pahali ambapo panastahili lakini isiingie katika vote nyingine.

Pia katika jambo lingine ni ya kwamba, kumekuwa na utumiaji wa pesa wakati wa kuhesabu watu. Iwe kwamba Chief aweze kuwa anajua watu wake. Hivi kwamba hata kama kuna mtoto ambaye anazaliwa, ni vizuri kwamba Chief aweze kuwa anajua hivi kwamba hakutakuwa na utumiaji mwingi wa fedha za Serikali. Ya kwamba kuna watu ambao wametumwa kwa ajili ya kuhesabu watu. Chief apatiwe jukumu ya kujua watu wa location yake. Na pia katika hapo, Chifu achaguliwe ambaye anajua kusoma na wananchi ambao wanamfahamu. Si Chief ambaye hajui kusoma kwa hivyo hataweza kujua hesabu ya kujua watu wake wako namna gani.

Ya mwisho ni kuhusu hali ya abiria wanaobebwa na magari kwa sababu sisi sote tunabebwa na magari ambao wale ambao wamepata magari wanatubeba. Hiyo ningesema ya kwamba, kuwe na sheria ya kusimamia abiria. Ya kwamba wengine

wanabebwa zaidi ya kiwango ya gari ambayo imewekwa. Kwa hivyo kuwe na hali ya kulinda abiria wanaosafiri. Ikiwa kuna wale ambao wamebebwa zaidi, ni vizuri hata hizo magari kuweza kuondolewa katika orodha ya uchukuzi.

Com. Bishop Njoroge: Wilfred?

Wilfred Kandawala: Asante Commissioners na wasikilizaji. Kwanza ningependa kuongea kwa upande wa elimu. Ningependa Serikali irudishe system ya zamani ya 7-4-2-3. Kwa sababu wakati huo wanafunzi hawakuwa na mzigo mkubwa vile wako nayo. Wakifika Form three, mwanafunzi alikuwa ana-specialize science. Halafu kuchukua career yake ilikuwa rahisi. Lakini saa hivi, wanabeba subjects kumi. Siku hizi hata akienda polytechnic, hata akifanya mtihani akipita, huandikwa kazi, ndio anaanza kuharibu kazi. Halafu tunarudi kulaumu Serikali.

Com. Bishop Njoroge: Can you recommend?

Wilfred Kandawala: Kwa hivyo, hiyo iwe. Tena Serikali ningetaka introduce mtihani wa zamani wa (inaudible) kwa wale yatima na chokora. Kwa maana hao wanahitaji ghalama nyingi na ni wengi sana wanataka usaidizi lakini hawana pesa. Kufikia form two, watapata certificate ndio wajiunge na wengine.

Administration: Upande wa Administration, Sub-Chief awe anachaguliwa na raia na villagers and the Chief by elders not the Government.

Employment: Any interview of the Government should be done in division headquarters, not districts to equalize Kenyans.

Second, any Government office should not have a majority from one tribe or one race. Asante.

Com. Lethome: Councillor karibu.

Councillor Mary Oluoch: Commissioners na watu wa Gilgil, karibuni sana Gilgil. Mimi yangu, kwa ajili ile ningeeonea, nimeona watu wengi wameonea na sijasikia mtu akiongea juu ya akina mama.

Com. Lethome: Ongea sasa.

Councillor Mary Oluoch: Akina mama tuko na shida kwa ajili sisi ni watu wanaume wanatupiga, tunachomwa na hakuna pahali tunaongea.

Com. Lethome: Wanaume ama waume?

Councillor Mary Oluoch: Waume.

Com.Lethome: Mabwana? Wajua ukisema wanaume bado huko barabarani kuna wanaume wanapita. Kwa hivyo kuna waume na mabwana.

Councillor Mary Oluoch: Sasa tunataka Katiba wakati huu iangalie maneno ya akina mama.

Com. Lethome: Ungependekeza nini kuhusu mwanamume anayepiga mwanamke?

Councillor Mary Oluoch: Ashtakiwe na afungwe.

Com. Lethome: Na wamama wanaoumiza waume wao?

Councillor Mary Oluoch: Hata wao washitakiwe na wafungwe. Kwa ajili wote wako sawa.

Ya pili, President wa Republic of Kenya, inatakikana tumchague from the grassroot na wananchi wote. Hata wakati huu wakati tunaenda kwa elections. Chama yeyote ambayo inataka kusimamisha President, inatakikana arudishe kwa grassroot kwa wananchi. Ndio ajue huyu ni mzuri ama ni mbaya. Instead ya kwenda kuchaguliwa na watu ishirini huko kwa Bunge. Kama itapatikana kiti cha Prime Minister, vile vile achaguliwe na Wananchi kutoka grassroot kama President.

Ya nne, land: Wanaume wanatisha wamama kwa land. Tunataka haki yetu, kama umeolewa na bwana amefanya na wewe arusi na anajua wewe ni bibi yake. Tugawane equally. Kama ni Title Deed, tuandike jina ya bwana na mama. Kwa ajili wakati bwana atakufa hatutakuwa na shida ya kuzunguka kusema, ooh niende Coast nirudishe mali ya bwana yangu.

Com. Lethome: Tafadhalini tuwe na mkutano mmoja. Tuna-interfere na recording na wamama (inaudible)

Councillor Mary Oluoch: Hayo maneno ya land unasikia?

Com. Lethome: Kwa hivyo Title Deed iandikwe jina ya mke na mume. Na wakiwa zaidi ya mke mmoja?

Councillor Mary Oluoch: Hata yeye agawiwe share yake.Wazee. Yuko Mzee mmoja aliongea hapa juu ya ukimwi na tunajua wazee ndio wanaleta huu ugonjwa wa ukimwi. Wazee ambao wako na pesa. Kwa hivyo watoto wetu wachanga kama tumetuma shule, wazee wananyemelea hao watoto, wanabeba watoto, wanawapatia pesa, wanawapatia ukimwi wasichana. Sasa kurudi wakati wa holiday, wasichana wanaenda kukutana na vijana wenzao wanapatiwa ukimwi. Sasa mimi naomba, wazee ma-sugar daddy ambao wanaenda kuchukua watoto wa watu kwa shule, akipatikana ashitakiwe na ahukumiwe. Kwa

ajili hawa ndio wameleta shida kwa nchi yetu.

Com. Lethome: Councillor unajua kuna sugar mummy?

Councillor Mary Oluoch: Hata sugar mummy. Wako sugar mummy. Wakipatikana na watoto wenzake. Kwa ajili hata mama amejua ako na ugonjwa na ako na pesa. Na yule mtoto fulani anatoka kwa family maskini. Yeye ananunua yule mtoto na pesa na anampatia ugonjwa. So, hata mama akipatikana, ashitakiwe na ahukumiwe.

MPs ambao wameongeza mishahara yao huko Parliament na hapa chini pahali wametoka, vijana wako na shida ya kazi. Hizo mishahara iwe reviewed. Tujenge nayo ma-factories, vijana wetu wapate kazi. Instead ya kuongeza MPs, pesa turudishiwe hizo pesa tujenge nayo ma-factories in our constituencies ndio vijana wapate kazi.

Haya maneno ya masomo ya MPs na Councillors. Hii ni kazi ya raia kwa ajili yule mtu ambaye raia ameona ni mzuri ku-represent wao, ndio wamchague. For example, mtu kama Kariuki Chatora. Alikuwa ni mtu hajui kuandika jina lake lakini alileta maendeleo makubwa sana Naivasha constituency. Unaweza kuwa na masomo, lakini kuingia hapo kwa Councillor ama Bunge, uweke mbwa kali kwa mlango.

Com. Lethome: Kwa hivyo masomo sio lazima?

Duncan Njoroge: Chairman, Commissioners. Nataka kuongea maneno ya kipande. Ukabila umeenezwa sana na kila wakati tunaimba ukabila shauri ya kipande, ID. ID ningetaka iandikwe bila kusema wewe ni kabila gani. Kwa sababu tukienda kwa ofisi wewe unajulikana ni kabila gani unaandikwa. Mwingine anawachiliwa. Kwa hivyo ikiwa kipande imeandikwa Kenyan kwa sababu ni mwananchi wa Kenya.

Com. Lethome: Unajua Mzee kipande haijaandikwa tribe ni form. Ile form inajazwa ndio iko na tribe lakini kipande yenyewe haijaandikwa tribe yako. Haijaandikwa tribe, ni form. Kwa hivyo form isiandikwe kabila?

Duncan Njoroge: Isiandikwe kabila, iandikwe jina la mtu tu na ni Kenyan. Ile ingine kazi, mtu asiwe na kazi mbili. Awe na kazi moja na aandikwe kulingana na qualifications za education yao.

Com. Muigai: Ngoja kidogo hapo Mzee, ni kazi ya binafsi au ni ya Serikali?

Duncan Njoroge: Ya Serikali. Kwa ofisi za Serikali.

Com. Muigai: Lakini mwananchi anaweza kufungua butchery na kufungua duka, hiyo hakuna shida.

Duncan Njoroge: Hata hiyo iwe limited. Kwa sababu tunalia kazi, watu wanalia kazi.

Com. Muigai: Kwa hivyo mtu yuko na butchery.....

Duncan Njoroge: Akiwa na moja, labda awe na mbili, lakini sio tatu, sio kumi. Mtu akiwa amejiriwa katika kazi ya Serikali ama ya public aharibu hiyo kazi au kuiba, ile mali amechukua ionekane amepelika wapi. Badala ya kufutwa anapelekwa transfer ama anafanyiwa kitu kingine.

Com. Lethome: Unapendekeza akipatikana afanywe nini?

Duncan Njoroge: Ashitakiwe na arudishe ile mali. Ama Serikali ichukue ile mali. Kazi ya polisi, polisi wanaenda kuchukuliwa bila kujua background ya yule mtu anachukuliwa. Ikiwa ni wakati wa kuwachukua hawa vijana kwa kazi ya polisi, Chief aulizwe kutoka area yake, kama anataka watu wawili, watu watatu. Chief anajua hao watu na tabia zao. Kwa sababu ikiwa mtu atakwenda kuchukuliwa na personality ile ako nayo wakati huo, huko nyumbani yeye ndiye huhangaisha watu usiku. Chief hatakuwa pale. Achukuliwe kulingana na recommendation ya Chief. Naye Chief mwenyewe awe amechaguliwa na watu kwa sababu watu wa area hiyo ndio watajua huyu mtu anafaa kutuongoza na ndiye ataleta wale watu watakuwa wakiendelea na kazi hata kwa Serikali kutoka area ile.

President asiongezewe muda wa zaidi ya vipindi viwili. Awe na vipindi viwili, awe mdogo ama mzee lakini isipite vipindi viwili. Tunaongea maneno ya President peke yake na Wabunge. Hata akipendwa namna gani, asiende zaidi ya vipindi vitatu. Kama ameenda viwili, ya tatu atakuwa amekalimisha ile kazi alikuwa anafikiria kufanya kama yeye ni Mbunge.

Ofisi za Serikali: Ningependekeza viwekwe masanduku, kila kitu nikiona iko makosa, naandika naweka hapo. Na itengenezewe wale watu, development board katika area. Wale watakuwa wakifungua hizo sanduku na kujua weaknesses za officer yeyote katika ofisi za Serikali.

Kuna hao watoto wa street children wanaitwa chokora. Wa leo ni watoto lakini kesho ni watu wazima. Hao watoto lazima wafikiriwe vile Serikali itafanya na hao watoto. Kwa sababu mtoto huyu akiachiliwa na awe mtu mzima, ile area ako hajui discipline ni nini, hajui nini. Ndio wanarudi kusumbua watu. Serikali ichukue hawa watoto wasionekane. Yule mtoto asikose wazazi wake, Serikali iwapeleke shule na wapatiwe primary education ili hata akiwa mtu mzima apelekwe hizi village polytechnics. Huyu mtu akitoka hapo hatashughulika na vita ama hatakuwa idle. Atakuwa na kitu cha kufanya.

Com. Lethome: Pointi nyingine.

Duncan Njoroge: Hiyo imetosha. Nimemaliza asante.

Com. Lethome: Asante sana. Njoroge Gichuki? Afuatwe na Peterson Kamau. Yuko? Atafuatwa na Jeremiah Muiruri? Peter Koilel. Paul Kamau. Joseph Mburu.

Njoroge Gichuki: Bwana Mwenyekiti wa kamati na wanakamati wa Tume na Wakenya wenzangu, yangu ni machache. Majina yangu ni Joseph Njoroge Gichuki na mapendekezo yangu ya kwanza, mimi ningependekeza tuwe na Serikali ya umoja wa kitaifa na wala sio Serikali ya Majimbo.

La pili, Bunge ama Serikali yetu ichaguliwe na wananchi kwa muda wa miaka mitano bali kusiwe na njia yeyote ambayo Bunge hili litajichagua lenyewe kama vile walivyokuwa wametarajia kufanya. Yaani pasiweko na nafasi ya Bunge kujichagua wenyewe.

Com.Lethome: Please Mzee, fafana kidogo.

Yaani kama vile Wabunge walikuwa wamependekeza Bunge lijiongezee muda bila kuchaguliwa. Kazi ya kuchagua iwe ya wananchi ama Wakenya. Bali si Bunge ikakaa kwa sababu kumepatikana jambo lolote ijichague. Isipokuwa tu kuwe na vita pengine.

Ya tatu, mali asili kama vile misitu ilindwe kisheria na isitolewe kwa watu binafsi. Kuwekwe sheria ambayo italinda mali asili ya Kenya kama vile misitu na isitolewe kwa njia yeyote ile kwa watu binafsi ama mtu binafsi.

Ya nne, nominated MPs na Councillors wachaguliwe kwa kipindi kimoja yaani wawe nominated kwa kipindi kimmoja kwa maisha ya mtu. Aki-nominatiwa kipindi hiki, baada ya miaka mitano tena, amekosa kufaulu, a-nominatiwe tena. Pia asiwe alikuwa amesimama uchaguzi akapoteza. Ningependekiza, isiwe ni yule alikuwa amesimama kwa Uchaguzi wananchi wakamkataa halafu pengine chama chake kionelee anafaa. Kama alikataliwa na wananchi, basi asiwe nominated. Kwa sababu ni kama kuwaudhi wale waliomkataa.

Ya tano, haki ya walio wachache ilindwe kisheria kwa kila eneo. Hapo ni kumaanisha ya kwamba, haki ya wachache hatuwezi tukaichukua, pengine nitumie mfano ya Wandorobo. Ya kwamba Wandorobo ni wachache ama Wa-elmoro ni wachache katika nchi. Lakini unaweza kwenda ukute, katika eneo fulani, Wandorobo ni wengi, kuna wachache katika eneo hilo.

Com. Lethome: Pendekeza.

Njoroge Gichuki: Kwa hivyo ningependekiza haki ya wachache ilindwe kisheria na Serikali.

Com. Lethome: Ya mwisho sasa.

Njoroge Gichuki: Ya mwisho, mashamba ya agriculture, research na mengine ilindwe pia kisheria. Na mwisho kabisa, adhabu ya kifo iondolewe katika sheria za Kenya. Asante.

Com. Muigai: Kidogo tu swali moja tafadhali. Kuna adhabu ingine isio ya kifo na ni ya kuchapa watu viboko. Hiyo ungeoneleaje? Watu wazima, wazee kama wewe na mimi, wanachapwa viboko jela?

Njoroge Gichuki: Corporal punishment ndio nimeonelea iondolewe kwa sababu kwa maoni yangu naona kama mtu akiuawa,

yule ametoa sheria....

Com. Muigai: Hiyo ni capital. Mimi nakuuliza corporal. Corporal ni viboko. Unaonaje juu ya viboko?

Njoroge Gichuki: Hata hiyo kwa maoni yangu ningei-term kama adhabu ya kifo. Kwa sababu haitakikani. Asante.

Com. Lethome: Joseph Ole Marui. Sasa kwa vile watu nawaita hapa na hawako, mtu yeyote ambaye sijamuita hapa na hajamzungumza. Ngoja tu, tutafuata utaratibu. Wajua hii kazi tumefanya miezi mitatu mfululizo, tumepata experience, tunaweza kufanya kama tumefunga macho. Hebu kujeni hapa hivi, wale wote wamejiandikisha na sijawaita. Wale wamezungumza wakae nyuma. Patrick nilimuita hakuwako. I called you, you were not here. Sasa tunaanza na wewe Patrick, halafu na huyu mama, halafu tukienda hivi. Kila mmoja atazungumza. Patrick halafu mama. Anza kwa majina. Na nikupendekeza tu.

Patrick Maina Kariuki: Jina langu ni Patrick Maina Kariuki, mkaaji wa hapa Gilgil. Chairman na Commissioners, pointi yangu ni kuhusu Uchaguzi. Mimi ningechangia na ningependelea, Uchaguzi usimamiwe na kikundi ambacho kimeteuliwa kutoka kwa makanisa na kutokana na wastaafu bali na vyama ama Serikali. Tena, Uchaguzi ufanyike mwaka huu bila kuunganishwa na Katiba kwa sababu Katiba ambayo inatengenezwa, Katiba hiyo ndio Kenya yetu kwa wakati ujao na hata kwa vizazi ambavyo tunatazamia, kwa hivyo isiunganishwe na Uchaguzi, eti ya kwamba ifanyike baada ya Katiba. Yaani baada ya Katiba kutengenezwa inaweza kufanywa haraka haraka na saa ingine Katiba ikose kusimamia hata watoto wetu, kwa hivyo Uchaguzi uendelee kama kawaida mwaka huu na Katiba iendelee mpaka wakati wa kumalizika kwa sababu hiyo ndio tutaitazamia.

Ninataka kuongea habari ya masomo. Shule zetu ambazo tuko nazo zimekuwa hivi karibuni ama siku zilizopita ya kwamba watoto wasichapwe na walimu na mimi naona ya kwamba walimu ni kama wazazi katika mashule. Pasipo kuadhibu watoto, watoto wamekuwa wakaidi hata hawezi kuwasikiliza walimu wao. Mimi ningependekeza viboko virudishwe kama zamani.

Com. Muigai: Vimerudishwa.

Laughter from the audience.

Wachapwe. Jambo lingine nataka kuongea habari ya traffic ama walinzi wa barabarani. Tumepata ma-accidents mengi sana barabarani. Tumepata magari malaghai katika mabarabara na tuna walinzi katika barabara na road blocks. Mimi napendekeza hivi, inaonekana walinzi walioko barabarani hawatimizi wajibu wao vizuri. Ingewezekana kama Katiba ikitengenezwa hata afadhali ipewe military police ambao wanachunga magari ya jeshi. Kwa sababu magari za jeshi mara nyingi hazifanyi makosa. Na kwa sasa, tukiwa barabarani pande zote hata pande za Lodwar, kila upande. Tunakuta traffic akiwa barabarani, kama hapewi pesa kwa mkono, inapelekwa nyuma ya gurudumu.

Com. Lethome: Nyinyi ndio mnawapatia?

Patrick Maina Kariuki: Ndio tunawapatia na inawekwa nyuma ya gari ama isitoshe inaangushwa chini. Kwa hivyo ingewezekana ipewe military. Na military inawezekana labda watafanya kazi nzuri na hayo mambo ya magari ipelekwe hata kama ni court. Tena mtu wa gari akishtakiwa, unakuta kama polisi hatapata rushwa, ikifika kule kwa Judge, ile karatasi inaenda inapasuliwa na mahakama ama kwenye kituo cha polisi. Kwa hivyo hiyo kesi haitaenda mbele. Kwa hivyo hiyo kesi ya magari, hata afadhali ipelekwe kwa jeshi.

Lingine nimefikiria limechangiwa na mwingine, lilikuwa ni habari ya silaha. Unaona watu wengi wanabeba silaha na wanasema kabila zingine ni kama watu wajinga hawajui kubeba silaha. Lakini sheria iwe ni kwa wote. Wote waache kubeba silaha na kama mtu atabeba silaha, achukuliwe hatua ambayo inastahili. Hata kama ni kuhukumiwa ahukumiwe na asibebe silaha yeyote ile.

Com. Lethome: Sijui unasema nini kuhusu mila za watu. Katiba ifanye nini kuhusu mila za watu. Ziheshimiwe au zisiheshimiwe?

Patrick Maina Kariuki: Nasema ya kwamba mila ziheshimiwe lakini sio kubeba silaha.

Com. Lethome: Na ikiwa kuna mila ambayo inasema mwanamume hawezi kutembea bila rungu.

Patrick Maina Kariuki: Sasa tuko katika Kenya, hatuko katika kabila.

Com. Lethome: Kwa hivyo ni kwa watu wote, hakuna kubeba rungu watu wote.

Patrick Maina Kariuki: Wote waachane na rungu.

Com. Lethome: Mpaka President?

Patrick Maina Kariuki: Hata President mwenyewe. Sina lingine.

Com. Lethome: Mama.

Deborah Wachanga: Majina yangu ni Deborah Wachanga. Commissioners na wajumbe wa Electoral committee na members nimewasalamia.

Com. Lethome: Although hatuhusiani na mambo ya elections ni Constitution.

Deborah Wachanga: Mimi yangu ya kwanza ni ya wanawake. Siku hizi wanaume wanatupa mabibi zao na akimtupa, pengine anamtupa na watoto. Akitupwa na watoto, anaambiwa aende. Mimi ningependekeza, ikiwa mwanamume wanaachana na bibi, ile mali iko kwa huo mji wao, iwe ikigawanywa mara mbili na watoto wawe wakigawanywa hivyo hivyo.

Com. Lethome: Watoto wagawanywe mara mbili?

Deborah Wachanga: Wagawanywe. Mama aende na nusu na baba aende na nusu. Na mali igawanywe.

Com. Lethome: Na wakiwa na mtoto mmoja ama watatu?

Deborah Wachanga: Huyo anaenda na mama kwa sababu Mzee hajui kuchunga.

Com. Lethome: Endelea.

Deborah Wachanga: Hiyo ingine ni ya wasichana. Vijana wanaweka wasichana wengi sana mimba na hawaulizwi. Nataka sasa wawe wakichukuliwa hatua. Ikiwa ni kufungwa, anafungwa kwa sababu ataacha hiyo tabia. Wawe wakifungwa kutoka miaka saba.

Com. Lethome: Wajua kitendo cha mimba, kinahitaji watoto hao wawili. Sasa huyu mmoja ndio amefungwa, na huyu mwingine achukuliwe hatua gani?

Deborah Wachanga: Mwanamke si unajua ataachiwa kazi ya kuchunga huyo mtoto. Kwa hivyo hakutarajia.

Com. Lethome: Lakini alishiriki katika kitendo hicho ama hakushiriki?

Deborah Wachanga: Si mwanamume ndio anakuanga na hicho kitendo, kwa hivyo mwanamume achukuliwe hatua.

Laughter from the audience.

Com. Lethome: Endelea.

Deborah Wachanga: Pombe: Mambo ya pombe ndio nilikuwa nasema, pombe yote imalizwe ibaki hii ya brewery peke yake. Pombe hizi zingine zote zikwishe. Ibaki ya brewery kwa sababu hiyo inaangaliangwa. Kwa sababu hizi zingine ndio zinaua watu. Hata chang'aa, hata busaa, hata mung'are, yote ikwishe, ibaki ya Kenya Brewery peke yake. Wazee wengine wanakataza

mabibi zao waingie kwa ma-group ya akina mama. Sasa ninataka wanaume wakubalie mabibi zao wawe kwa ma-groups za akina mama.

Constituency hii yetu ya Naivasha ni kubwa, ningependelea ipasuliwe mara mbili, iwe Gilgil na Naivasha. Siku hizi tuko na shida ya mapolisi, ukiwa na shida uende ushitaki kwa polisi, hawezi akakuandikia shida yako kabla hujatoa pesa umpee. Hata kama pengine kuna mtu amekataa na pesa zako kama shilingi elfu moja. Naye ili aende aitishe, anakuitisha elfu moja, sasa unaona shida imeingia. Hata hiyo elfu moja tena akiletewa, anakwambia ukuje leo ama kesho. Ukija anasema haijafika na ikikuja anasema 'hukukuja siku ile nilikwambia.'

Com.Lethome: Unapendekeza nini ingawa, kuna kazi ya polisi na ya jeshi. Sijui unapendekeza nini?

Kuwe na raia wale watakuwa wakiangalia polisi kwa sababu wako na mashinda. Wawe wakichaguliwa na watu, wanaenda police station, wanaona vile wanafanya. Tunaambiwa Kenya tuko na uhuru wa kuabudu lakini huo uhuru wa kuabudu umezidi. Sasa, mimi ningependekeza ya kwamba ile kanisa ambayo haijakuwa registered kwa Attorney General, yote ikwishe, ibaki ile registered. Yangu ni hayo tu.

Com. Lethome: Asante sana Mama. Sasa tunaanza kufuata mlolongo wetu. Dakika tatu, tatu, kila mmoja azungumze. Anza kwa majina yako.

Bernard Mutava: I am Bernard Mutava, I have got several proposals to make to the Commission. First is on education, that is we should scrap the 8-4-4 system and come up with the 7-4-2-3 system and also pertaining the education, we should have the Higher Education Loan Board. The Higher Education Loan Board should give provision for Polytechnics because currently it touches on the Universities alone. So, the Polytechnics should be considered as well.

Another proposal pertains the Judiciary: We should have a fair and transparent Judiciary. Currently, in Kenya people believe that, why hire a Lawyer, while you can buy a Judge. The Judiciary should be made fair and transparent. By this I mean that whatever has been said by the Judiciary should be subject to review and the A.G. should also not be final when it comes to Judiciary. He should be subject to questioning whenever he passes.

Then another one is on the tourism sector. One thing you know that the already obsolete Constitution did not provide for the tourism sector as much as it should be. For example, the tourists are highly taxed in Kenya as compared to some other aspects in the country. Also, something like the (inaudible) should be scrapped out and this I mean that fair prices should be given to tourists as well as the normal Kenyans. For example we have had cases of tourists complaining about being highly charged and also there should be a Constitution governing their security as well. Cases of may be the tourists being mis-handled and mis-treated in Kenya should be addressed by the current Constitution.

Also, the State organs should be bureaucratically merited and by this I mean that we should elect the right people to occupy the right offices. It is very unfair to come up with a person who learned about agriculture to man the Financial Ministry, so they should merit those offices as they deserve. This will also reduce the Presidential nomination powers. Because the President currently can nominate anyone to rule any organ of the State, which is not fair.

Lastly, I would like a particular Section of the current Constitution and that is Chapter 208 of the Kenya current Constitution, it deploys that the law of the Act that currently exists, it doesn't give provision for Student's Act. I don't know whether I am clear when I speak of Chapter 208 in the current Kenya Constitution. It should be reviewed and also provide for the Student's Act.

Secondly, the mileage rate that stipulate today that is eighty cents per mile should be updated as well because that one is not realistic and also the allowances thereby addressed to, the (inaudible) should as well be reviewed. I think those are my views.

Com. Lethome: Next.

Harrison Waweru Ng'ang'a: Mimi kwa majina naitwa Harrison Waweru Ng'ang'a na mimi Chairman wa Katiba nitatoa maoni yangu kuhusu hawa watu wanaitwa wachungaji wa kuhamahama. Hawa wachungaji wa kuhamahama, saa ingine wanaenda wanadhuru wale ambao wanakuta. Kwa sababu wakati wanatoka kikao chake, anaenda, anakwenda kukaa katika kikao cha mtu mwingine. Na wakati anaenda huko, anaenda kuishi kwa shamba ya mtu yule amemkuta hapo.

Com. Lethome: Sasa unapendekeza nini?

Ningependekeza huyo, awe akipewa kama ni mtu huyo wa kuchunga, akimaliza wiki mbili anaondoka anarudi mahali alitoka.

Tena ya pili, kuna mambo mengine inatendeka katika nchi hii yetu. Mtu anakuja anakamatwa na akikamatwa kufikishwa huko kwa polisi, unakuta mwingine anawekwa rumadi siku kumi. Mwingine anawekwa hata kama aliua, anaenda kuwekwa miaka tatu.

Com. Lethome: Unapendekeza nini?

Napendekeza mtu yule atazidi, awekwe rumadi kwa muda wa wiki tatu. Kesi yake iamuliwe aondoke aende. Kama ni kufungwa afungwe. Tena katika area kama hii tunakaa, kila mahali iko hospitali kubwa iwe na mortuary. Kwa sababu watu wanakufa na mpaka umtoe mtu hapa umpeleke Nakuru, na utamrudisha Gilgil. Kila mahali iko hospitali na iko town, iwe na mortuary ya kuweza kuhudumia wale watu wanakaa pale. Asante Bwana Mwenyekiti.

Com. Lethome: Next.

Bwana Commissioners, Chairman wa Commission, kwa majina yangu naitwa David Mutegi na ninagombea kiti cha Nakuru na maoni yangu ni kama yafuatavyo. Ya kwanza, ningependekeza ya kwamba katika every constituency registered voters wawe not more than fifty thousand. Na pia ningelitaka kwamba President anayesimama na kuchaguliwa, tusiongee mambo ya twenty five percent but we talk about fifty percent. Yaani awe na nusu ya watu ambao wamempigia kura. Isiwe inamaanisha ya kwamba lazima apewe kutoka Provinces.

Pia katika maoni yangu ningelipendekeza hivi Bwana Commissioners, ya kwamba sheria, President asiwe above the law na pia muda wa Parliament uwe katika mikono ya wananchi wa Kenya wote kujua tarehe za uchaguzi. Na wakati wamechaguana wajue the next election itakuwa wakati gani. Isiwe ya kwamba hayo ni mamlaka ya President, kuzungusha Bunge ama kuivunja wakati anapotaka.

Pia, Bwana Commissioners ningewauliza, mali ya wananchi ama mali ya mtu binafsi iheshimiwe na sheria I-guarantee. Lakini sio vile mambo inavyofanywa kwa sasa kama ya kwamba, inakuwa, sheria zinavunjwa na watu wengine wakivunjiwa sheria sio kama sheria imevunjwa.

Bwana Commissioners pia ningelitaka kusema mambo ya ardhi. Sheria za nchi hii kuhusu ardhi zimekuwa sheria za kutaabisha sana na hasa zimeweza kufanya wananchi wengi kupoteza mashamba yao na hata kuumia katika mikono ya walaghai hasa katika zile zilikuwa kama land buying companies. Ambapo wale waliokuwa kama ndio Ma-Directors, walitumia mamlaka yao na wakaharibu kila kitu. Kwa hivyo ningelitaka iwe hivi, kwanzia sasa iwe kama ni haya yote mambo, yachunguzwe kutoka sehemu moja, kama ni ile ya division kama Gilgil, pawe na mtu ambaye anaweza kuwa answerable na iweze kufuatwa hivyo. Kwa sababu kesi hizo zikiingia kortini zinachukua hata miaka nenda rudi bila...

Ningeuliza pia vile mambo inaendelea ya registration of voters, isiwe ni kitu ambayo inafanywa kwa siku moja ambapo inaachwa tena katikati mpaka tena iwe itaambiwa ni siku gani. Iwe ni kitu ya kuendelea kwa sababu kuna watu wengi wanapata vipande kama leo, na kesho watatakiwa wapige kura. Kwa hivyo ningelitaka vipande na kura zinaenda pamoja.

Bwana Commissioners pia ningelitaka kuuliza kitu moja, sheria zetu pia kwa upande wa akina mama ningelipenda kupendekeza kitu kimoja. Kumekuwa na shida kubwa hasa za rape cases ambapo wengine wanashika wengine kwa nguvu na mambo kama hayo. Mimi ningeuliza mtu yeyote anayehusika na mambo kama haya, sio kuchukuliwa tu hatua rahisi, iwe hata kama itafika mahali awe ni kuwekwa ndani maisha. Iwe ni hivyo. Ama hatua kali zaidi ya hiyo kwa sababu hicho ni kitu kinaendelea na wengine wanafanya hivyo wakiwa na maradhi kama ukimwi na vitu kama hivo. Kuna kitu kingine pia ningetaka kusema, mambo ya Jua Kali Bwana Commissioner ambayo inahusu mambo ya nchi yetu kwa sababu ya ukosefu wa kazi.

Ukosefu wa kazi na Jua Kali, Serikali ingestahili zaidi kulinda Jua Kali zetu ambazo zinaamka na especially viwanda vidogo vidogo ambavyo ndio ilikuwa mwongozo wa Serikali ilipoanzisha Ministries kama vile Science and Technology. Ikaanzisha Wizara kama ya Biashara ndogo ndogo na vitu kama hivyo, lakini imekuwa ya kwamba haikufuatwa kwa sababu utakuta vitu vingi vinatoka kutoka nje baada ya liberazation. Tung-liberalize vile vitu hatuna lakini vile vitu tunavyo hapa kwetu, tuone vile tunaweza kuendeleza viwanda vyetu ndio vijana wetu wapate kazi.

Com. Bishop Njoroge: One minute.

Mahakama kuu ningelipenda iwe hivi, kukisha kuwa na mahakama inasikiza kesi hata kama ni mahakama kuu, kwa sababu kesi unaweza kukuta mahakama ndogo imekubali, sheria imevunjwa. Kwenda high court imekubali lakini ikifika katika ile court of appeal, inasemekana haikutumika vizuri. Sasa ningelitaka hivi, baada ya hivo iwe, badala ya kuitupa hiyo kesi, inarudishwa kwanza, ichunguzwe upya ili ionekane kwa sababu watu wengi wanapoteza mali zao kwa sababu ya zile corruptions zinapitia huko juu. Kwa hayo, sina mengine ya kusema.

Councillor Mureithi Mutahi: Bwana Commissioner mimi naitwa Councillor Mureithi Mutahi kutoka Karuga location hapa katika division hii ya Gilgil. Sina mengi kwa sababu mengi yamesemwa lakini ningegusia tu kwamba, katika Katiba mpya Machifu wanastahili kuondoka na kuwa-replaced with an elected leader.

Ya pili ni mambo ya harambees, zimekuwa highly abused na katika Katiba mpya ningeluliza zitupiliwe mbali kabisa na kama kuna high hospital bills, kunazo zinakujanga high hospital bills they should be discovered by the Central Government from the public treasury.

Mambo ya extension ya Bunge inastahili kufanyika kulingana na Katiba ya sasa wakati nchi iko na vita. Lakini katika Katiba mpya ninguliza iwe extended. Even when the country is undergoing constitutional review like now. Kwa hivyo hata sasa tukienda na hiyo iwe-extended hakuna shida.

Mambo ya Presidential powers zitarudia, yamesemwa mingi sana. Mambo ya Councils, Councillors do not control County Councils, huwa controlled by the Kanu Government through its chief officer. So, hawa Chief officers waondolewe na iwe shared by Councillors. Councillors wa-control Councils.

Ile ingine ni mambo ya vyama. Visiwe vyama zaidi ya vitatu. National resources, people should own land, only the land they can utilize. But not like now, from Naivasha to Nakuru it's one person. Mambo ya hanging iwe abolished, iwe life sentence. Iwe religions na cults. Haya makanisa yote yamekuwa ya kibiashara, kutengenezwe Ministry of Religious affairs. Ikatwe kidogo, kukuwa mingi mingi ya kibiashara.

Lingine ningengeza ni haya mambo ya Ardhi Houses all over the country, have become so corrupt. Mambo ya mashamba iwe handled ama any kind of land should be handled by the County Council.

The final point ni mambo ya nominations ya MPs na Councillors. Nomination while in political parties. Hiyo, tukae na elected leader. An elected MP or an elected Councillor. Nomination ya members to the Parliament and Councils ni mambo ya kupoteza pesa za Serikali kwa hivyo tukae na the elected ones. Asante.

David Mburu: Wanachama, Chairman na wanakamati. Ninaitwa David Mburu. Ningetakia vyama vya siasa viwe tatu. Chief achaguliwe na watu. Itakuwa kitu ya manufaaa. Mayor pia achaguliwe na watu. Kuhusu pombe mimi ningependelea pombe kama busaa iwe free. Kwa sababu kuna wazee wako huko nyumbani na wanataka kukunywa, hawawezi kuja kwa bar akunywe bar. Kwanzia saa nane mpaka saa kumi na mbili, mnafunga. Kuhusu Uchaguzi, mimi ningependelea Uchaguzi ufanywe mwaka huu lakini Katiba iendelee kurekebishwa. Ni hayo tu.

Julius Gichira: Kwa majina naitwa Julius Gichira. Yangu, yale ningesema yamesemwa yote lakini nitarudia hata mengine. Maana kama kuna ingine nikiwa siko.

Com. Bishop Njoroge: Mzee, sasa unapoteza wakati wako.

Julius Gichira: Napoteza wakati. Sasa ningesema kuhusu mashamba. Mashamba kubwa kubwa, yote yalilaliwa na Wazungu. Na Mkenya wa kawaida na sheria ziko, hata yeye angepunguziwa kidogo wananchi kadha wa-squeeze kwa hili shamba lake. Kama Delamere kutoka Nakuru mpaka Naivasha ni yeye. Na hilo shamba hakununua ni shamba alinyang'anya watu hapa. Ni unyakuzi huo, kunyakua. Hata haya mashamba, tunasema makubwa, makubwa, madogo, na hatupati. Habari ya mashamba iangaliwe. Mashamba makubwa makubwa.

Tena nintaongea jambo la pili kuhusu kazi. Kazi kuajiriwa, inakuwa kama ni kabila moja ndio inakuwa ndio majority kwa kazi. Kama mkubwa yuko hapo kazi. Hata kama kazi ya jeshi na imeandikwa kila mahali. Unasikia mtu anatoka Rift Valley, anabebwa na gari usiku kwa maana anajulikana...

Com. Bishop Njoroge: Can you recommend?

Anaenda kuandikiwa tuseme Mombasa kwa maana huko ndio kuko na recruitment. Kwa hivyo sasa hiyo iangaliwe kama kuna watu wa kuwafuata nyuma. Wakujua kama walifanya vizuri. Wasifanye vile walifanya Nakuru wakakuja kuita watu majina na wananchi walikuja. Huo upande wa kazi kuandikwa imeenda tofauti tofauti.

Inginge nakuja sasa upande wa shule ama masomo. Naonelea Standard Seven ile ya zamani irudishwe badala ya Standard eight.

Na masomo vile inasemekana iwe ni free from Form one to Form four. Maana hata hii Primary (inaudible). Hiyo nayo hapo imechangia. Masomo iwe free kama itawezekana kwa Katiba mpya.

Jambo lingine natilia mkazo hata huyu alikuwa hapa ameongea na hata mimi nitaongea. Kuna pombe: Wakati kulikuwako na pombe ya busaa, hata yule mtu hana nguvu angeweza kununua busaa yake ama anunuliwe na mtu mwingine kwa maana ilikuwa ni bei rahisi. Hata mama akipika busaa, mtoto wake hawezi kufukuzwa shule, pesa atapata hapo nyumbani. Kwa hivyo iwe free to the whole country. Sio vile ilisemekana ifungue. Tuwachiliwe, yule ataweza apike. Na tena kama vile tunazidi kugundua madawa ya miti ni dawa, tangu hata kabla Mzungu kuja hapa tulikuwa tunatumia miti ya misutini na tunaponya magonjwa.

Com. Bishop Njoroge: Kwa hivyo una-recommend miti ni dawa?

Lakini sasa tunasikia kuna district moja inafungwa sijui ni sheria gani hiyo. District moja inafungwa, district ingine iko na miti ni dawa na inasaidia wananchi. Hiyo ningeonelea miti iendeleo ni dawa na pombe ya busaa. Kuongea mambo ya employment, iwe equal. Hiyo nimeongea na nafikiri hakuna shida nafikiri umeelewa.

Com. Bishop Njoroge: Pointi ya mwisho.

Tunakuja kwa sheria ingine, hii sheria ya wizi wa ng'ombe hii 278, ya penal code. Hiyo irekebishwe kwa maana yule mtu anaiba ng'ombe yako na anachinja huyo anafungwa miaka kidogo na yule anakamatwa na ng'ombe red handed na ng'ombe ile haijakufa, huyo ndio anagongwa miaka saba. Sasa unaona hapo, hii sheria ilichukuliwa namna gani. Hiyo 278 ingerekebishwa. Hata yule ameua ng'ombe ndio angefungwa ninety. Hiyo sheria naona hapo iko tofauti.

Kuna ingine nitachangia hapo. Kama unaona vile Zimbabwe nini na nini, isije ikaingie hiyo ya mashamba ya Wazungu, tuangaliwe na hiyo ni kukuambia urekebishe hapo. Sasa hii tumebaki na hii yetu Title Deed. Kama mimi kwetu ni Meru. 1968 ndio mashamba ilipimwa. 1967-1968, mpaka wa leo hatujapata Title Deeds na mtu alipasuliwa yake. Hiyo sheria

Com. Bishop Njoroge: Can you give recommendation? Title Deeds zipeanwe?

Title Deeds, mashamba ikimaliza ipeanwe. Waache kutueka.

Com. Bishop Njoroge: Can you give us your last point please? Pointi ya mwisho.

Pointi ya mwisho ni kuhusu pesa ambazo zinakatwa na Serikali, kodi ya mapato. Hii kodi ya mapato pia tunapeana na pesa haturudishiwi, inatumiza. Na tena hii ya Hospitali. Hii ya Hospitali yaani N.H.I.F. haijangu kitu. Kwa hivyo nilionelea hapo tunafinywa sasa. N.S.S.F. pia. Ikiwa ni kiwango kama mtu amefikisha hata kufikisha miaka hamsini hiyo, wanasema

tupunguziwe. Naona umeniharakisha, I had more to say. Lakini

Com. Bishop Njoroge: No. You have utilized your time, we are going to read the memorandum. Kwa hivyo mupatie mtu mwingine chance.

Fredrick Gachemi: Bwana Chairman, Commissioners na listeners. Jina langu ni Fredrick Gatiba Gachemi. Na ni na haya ya kuchangia. Ya kwanza nasema habari ya Kenyan labour. The Kenya Government has not seen the way to remunerate the labour according to the productivity and this is ranging from private sector to civil service. So, there should be a remuneration measure. Let me also visit the issue of Kenya Gazette (inaudible) order. This order, that the Government do issue, once it is issued it is always below the level on the ground. So, the Government does not do a realistic remuneration. If you check the order on the ground today, it does not appear anywhere factually. If anything that the Government should do, should become a model example if not the best.

Another one, Kenya Domestic Productivity that is E.D.P. If the country's labour force is economically empowered, the taxable people will automatically increase, hence more Government revenue collection. When you visit the issue of employers and employees, this is on private sector now. The Government has made rules, it grips over the employer. Because on the ground workers are crying. Because labour cases are taking years to arrive to a solution. The other point, by luck the employers have gone ahead in saying that, 'your Government is in my pocket.' What do I imply about this? All of them are under my shoes. So, this brings the worker to a zero or any other frustration. So, what the Government should do is to emphasize the rule of law. Nobody should be above the law. This situation makes it harder for workers union to harmonize the labour private sector.

On the civil service, the Government has it in his hands. So, it should harmonize it accordingly. On the issue of Kenya's economy. Taking it from the ground, there should be a creation of centralized revenue collection. There should be a board.

The other point is creation of enterprising environment. That is associations should be encouraged, mobility of entrepreneurs and law guiding those particular factors. Low taxation should be given to create more taxable entrepreneurs.

On Agriculture, you will find that it is actually crowded, so farm inputs should be given the least tax or zero tax. Tax collection should be harmonized so that the revenue collection is done otherwise, the business world has brought the Government to its throat.

On Presidency, he should not be above the law and let there be a Governance that is conducive to allow good delivery. Judiciary, it should be free from any quarter. It should be independent. On Public services, there should be the right person for the right position as it is in private sector. When we come to Parliamentarians, they should be lead through a regulatory board. Asante.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much. Those were good points.

Harrison Ngaratia: Jina langu ni Harrison Ngaratia. Yangu ni machache, ni kuhusu uongozi, pande moja nasema kwamba, mtu akichaguliwa kuwa, yaani the President anataka kutengeneza Serikali, Cabinet Ministers lazima wawe vetted. Isiwe the other way. Awe vetted thoroughly. Pointi hiyo ni kwamba elections, wasikubaliwe kuwa nominated. Hiyo ni kusukuma wengine viti. Kwa sababu umemshinda na anasema eti umenishinda. Tayari umekuwa nominated. Kwa hivyo, a loser asikubaliwe kuwa nominated.

Upande mwingine, jamii: Jamii, kuna watu ambao wanashikisha wasichana wetu mimba. Na ningependa hao watu waajibike. Akipimwa na daktari aonekana ya kwamba yeye ndiye amemshikisha msichana mimba yule. Awajibike mpaka miaka kumi na nane. Na iwe inaangaliwa, sio aajibike tu kwa maandishi. Lazima iwe anaangaliwa anatumza huyo mtoto. Upande mwingine tumekuwa na ugonjwa wa ukimwi kwa wingi sana hapa na ni jambo ambalo hatuwezi ficha. Imekuwa aibu sana kuona wasichana wetu wazuri wanafaa nguo za kubana zaidi. Na hiyo hakika hata kama wewe ni mwanamume, ni kweli kabisa inachangia mambo hayo ya rape. Inachangia. Kwa hivyo nguo ziwe za kiheshima. Lazima kuwe na nguo za kiheshima.

My last point is town planning, I am a masion*, najenga hapa Gilgil, hapa Gilgil kwa mfano, hakuna hata park ya kupumzika. Nikikwambia uende upumzike, hakuna. Watu wame-grab hata barabara zimeisha zote. Ningependa Serikali ambayo inakuja ijaribu kuweka in order ili angalao mtu akisikia amechoka anaweza kupumzika kwa miti. Hapa hatuna. Thank you.

Simon Waititu: My name is Simon Waititu or Sudai, and I would like to present my views....to give my pillar of concern not only to me but to my fellow citizens, especially a matter of religion and public schools. Rule of unconstitutional practise of reciting prayer a non-denominational prayer in public schools should be banned. It should also be forbidden, religious tongues, religious instructions in public school buildings. Because our country is so diverse with so many religions of different backgrounds. I also understand that we have freedom of religion. So, we can expect the same authority which has established such a law at the same time to sideline or promote one religion and at the same time dis-regard others.

Also, I propose that there should be a clause which should rest upon on awareness of the historic fact that Governmentally established religions and religious perpetuations be covered in Act. I would like also to talk about freedom of speech and (inaudible). A perennial problem of civil liberty is that of reconciling freedom of speech unutterably with the authority of State, to protect and preserve public peace and order and tend to administer and enforce the same (inaudible) with individuals who sometimes try to emphasize their constitutional rights. May be addressing of topics which they feel, there is no way they can put it. So, I think the Government should clearly explain or put it into law, to what extent can we say that people should not be free to address or assemble together in a gathering. And what makes it a crime? Because as you can see.....

Com. Bishop Njoroge: Since, you have explained. Just make your recommendation.

So, I would like to recommend that the Government should rule out laws that are very clear on the matter. Freedom of expression absolutely. Another thing is about obscenity and freedom of expression. We see in our country we are getting obscenity and freedom of expression. Everytime we are seeing a lot of phonographic material being provided through literature and audio visual. Recommendation is that the Government should come up with clear laws or a (inaudible) which is sensitive to our traditional morals so that we can avert the polluting of our youths mind through such literature and importation of such materials. I would also like to talk about internal security, the Government has the right to check movements which they think are dangerous to the society but at the same time, there should be clear and fair judgment about guilt of association. How can we say a person is guilt of association and may be in case of (inaudible), he was just answering orders from a superior. So, I propose that kama hii sheria ya treason iwe abolished na all citizens wapewe equal laws ambazo zinangalia jambo hilo.

Shida ingine inahusu Land and Agricultural policy, Serikali iwe na sheria ambazo zinaonyesha juu ya haki ya watu kumiliki land in our country and also agricultural policies which are sensitive to our rights. Hivi kwamba, Serikali inapaswa ku-provide not only the land but even the insensitives to develop that land.

Com. Bishop Njoroge: Final point.

The final point ni kwamba, social services na institutions ambazo ni already established ziwe overhauledand re-structured ili ziwe responsive na sensitive to mahitaji ya Kenyan citizens, workers and children's welfare. Kama N.S.S.F, ijali watu wote dis-regarding where they are in Kenya. Whether mtu ako Turkana and he doesn't work. He is a Kenyan citizen. Ana-deserve income, ana-deserve medical care, na watoto wake, hata education. Na hizi institutions zinapaswa kuwa pyramid ili ziweze ku-address such issues.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much.

Seleiyo Ole Ndemeru: Asante Bwana Commissioner. Kwa majina ninaitwa Seleiyo Ole Ndemeru na mchango wangu wa kwanza ni kuhusu Uchaguzi. Tunataka tufanye uchaguzi bila Katiba ya sasa. Tufanye Uchaguzi kwa Katiba tuliyo nayo sasa, mwaka huu.

Ya pili, nachangia mambo ya kitambulisho. Kama sisi wakaaji wa hapa Gilgil. Sana sana jamii ya Wamasai wapate kitambulisho. Sijui Serikali ilitoa sheria gani ya kukataza watu kama sisi Wamasai wa Narok huko. Tuseme hata Rift Valley, hatupati vitambulisho. Kama vile tunaishi hapa, tuko watu wengi ambao hawana vitambulisho na hata kura hatujapata kwa sababu ya vitambulisho. Ningetaka hiyo iangaliwe kama ni sheria, hiyo sheria irudishwe kama zamani, tupate kitambulisho ili

vijana wetu waweze kupiga kura. Kwa sababu kama sasa tuko zaidi ya watu mia mbili, wako hapa Gilgil au mia tatu, hawana vitambulisho na hawezi kupiga kura. Tunataka hiyo iangaliwe sana.

Ya tatu, ni mambo ya mila. Mambo ya mila iheshimiwe. Kama sisi ni watu wa kuhamahama. Na kama wakati wa kiangazi tunahama hama, watu watambue ni kazi tunafanya. Hizo ng'ombe tunahamisha hamisha namna hiyo ni mali ya Kenya, watu wote wa Kenya wanatumia hiyo mali na watambuliwe. Kama sasa wakati wa kiangazi tupewe nafasi kila mahali. Isiwe shamba, mtu hajafence, ng'ombe iende hapo, itembee ikule nyasi na irudi kwao. Hiyo nataka itambuliwe.

Ya nne, tunasumbuliwa sana na mambo ya kanyanga. Kama Wazungu wako hapa. Yuko mmoja anaitwa Marura na mwingine anaitwa Delamere. Hawa Wazungu walinyakua mashamba, hawajanunua, ni kunyakua wamenyakua na tunataka watambue sisi ni wananchi wa Kenya. Kama mtu hajanunua hili shamba amenyakua, tunataka huyo mtu atumbue sisi ni wakaaji wa Kenya, atupatie nafasi, tupitie hilo shamba lake. Kama ni maji tunaenda kutafuta tupate maji, na atambue sisi ni Wanakenya. Kwa sababu anashika sisi anatupeleka kortini na tunatoa fine.

Ya tano, ni kuhusu mambo ya ulevi. Kama mtu amepatikana usiku na polisi. Anashikwa anapelekwa, anawekwa cell. Kesho anapelekwa kortini. Hiyo mimi ningesema namna hii, hawa polisi wanapata mtu ameelewa, hajafanya makosa, aeke fine na kesho aachiliwe aende nyumbani. Kwa sababu hakuna makosa amefanya. Awachiliwe na kesho yake aende nyumbani.

Jambo lingine langu la mwisho ni hili, ningetaka kama akina mama. Mamlaka ya akina mama isipite ya mzee. Mamlaka ya akina mama iwe tu, mama yuko chini ya mzee. Sisi ni Waafrika hatuwezi kuiga mambo ya Wazungu. Akina mama wawe chini yetu na Mzee juu. Na Mzee juu. Hilo ndilo jambo langu la mwisho.

Com. Bishop Njoroge: Points points. Taja jina lako.

Danson Maina: Mimi naitwa Danson Maina, mkaaji wa hapa Gilgil na mimi ni mtu wa biashara. Ningependa Katiba ile tunaendelea kurekebisha, ya kwanza yangu ningenelea ni Presidential powers. Hiyo ndio imeleta watu wanajiita godfathers. Anasema mimi nimeongea huko juu. Ningependa hiyo iondolewe, President asiwe na powers, powers ziwe kwa Bunge.

Ya pili, ningetaka Ma-Judges wa Kenya ambao wanakata kesi, wawe appointed kutoka kwa Parliament. Parliament inaketi ina-appoint Ma-Judges ambao ni wale qualified.

Ya tatu, Attorney General awe akipata powers kutoka Parliament. Kama ni kesi ya mtu au ni mambo ya kisheria itoke kwa Bunge.

Ya nne, ningependa Ma-Chiefs na manaibu wao wawe wakichaguliwa na wananchi wenyewe. Kwa sababu wananchi

wenyewe ndio wanajua huyu ni nani na huyu ni nani.

Ya tano, kikosi cha polisi kimekuwa na utovu wa nidhamu kwa wananchi wenyewe. Tunataka the new Government, Serikali itusaidie kama kuna askari ambao hawajahitimu kutoka kwa training. Kwa sababu kuna wengine wako wanafanya kazi na hawajahitimu. Warudishwe ndio wawe wakijua sheria ni nini. Akishika mwananchi anajua ku-handle mwananchi hata kama anampeleka cell, awe akijua ni kesi gani. Mambo ya kupiga mtu akiwa kwa cell, hiyo Serikali iangalie sana kwa sababu watu wengine wameumia zaidi wakiingia kwa cell.

Ingingine ni upande wa security. Mimi binafsi nikiwa hapa nina uchungu, ningependa Serikali ichukue jukumu la kupigana na wakora. Kwa sababu mimi nimehama kwangu shambani, nimekaa kwa town na nimehama kwa sababu ya kupigwa na wakora. Hiyo security hatuna na kama tuko na Serikali, security inaweza kosa kwa sababu gani?

Ya mwisho, ningependa tena mtu aki-defect, mambo ya defection, mtu akichaguliwa kwa chama fulani na anataka tena kuhamia chama kingine. Sisi wananchi tumeumia kwa sababu hizo pesa zimetumika kuenda kufanya uchaguzi mwingine, zimetoka kwa kodi ile tumetoa kwa mifuko yetu. Kwa hivyo sisi tumehangaika na hizi kodi zinazoongezwa kila mara. Kwa hivyo kama hakuna defection, Serikali haingetumia kiasi kubwa ya pesa. Kwa hivyo tungependa mtu aki-defect anakaa miaka mitano mpaka tuchaguane tena. Lakini tumekubali, kama mtu akifa, wananchi wanatakiwa wa hiyo area....

Com. Bishop Njoroge: Unasema mtu aki-defect, asikubaliwe kusimama kwa miaka mitano?

Danson Maina: Kwa miaka mitano.

Com. Bishop Njoroge: Saa hiyo ofisi ikae hivyo na hicho kiti....

Danson Maina: Na hicho kiti kikae hivyo. Lakini akikufa, wananchi wapatiwe hiyo nini.

Com. Bishop Njoroge: Njoo hapa Mzee ujiandikishe.

Peter G. Muya: Commissioners, I also have something to say. My views, one is on Chiefs. My name is Peter G. Muya. The first one is Chiefs and Assistant Chiefs. They should be transferable like any other officer as it was before. We have K.W.S. Today, you find that animals are more respected than human beings. If a human being kills an animal, he can be jailed for so many years. If an animal kills a human being that is nothing. Therefore, we want to say that the compensation that was there which was about thirty thousand should be increased to about half a million. If a person is killed by an animal. That includes, crops destruction by wild animals.

